# ELLEN WHITE PRE AND PRIMARY SCHOOL

**P. O. Box 3118, Nzuguni Dodoma – Tanzania**

**Mob: 0769 352 215 / 0673 443 962**

**Email: info@ews.sc.tz Web: www.ews.sc.tz**


**Kumb. Na. EWS/PNA/2026/02** **29/07/ 2026**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Ofisi ya Meneja wa **Ellen White School – Dodoma**, inapenda kutangaza nafasi za kazi (4) za kada mbalimbali ili kuimarisha utendaji wake. Watu/Watanzania wote wenye sifa na uwezo wanaalikwa kutuma maombi yao ili kujaza nafasi za kazi kama zilivyoainishwa hapa chini:-

### 1.0 Mhasibu Daraja la kwanza I A – Nafasi 2

#### 1.1 Majukumu ya Kazi

(i) Kupokea na kurekodi michango na ada za wanafunzi shuleni

(ii) Kudhibiti matumizi, kulipa Ankara za watoa huduma na kusimamia manunuzi madogo madogo ya shule.

(iii) Kuandaa makadirio ya mapato na matumizi kwa kushirikiana na Mwalimu Mkuu

(iv) Kutunza vitabu vya fedha na nyaraka zote za kibenki kwa usahihi.

(v) Kuandaa taarifa za fedha kila mwezi na kuwasilisha kwa Mwalimu Mkuu paonja na Meneja wa shule

(vi) Kusimamia na kuandaa malipo ya mishahara ya walimu na wafanyakazi wasio walimu kwa wakati.

#### 1.2 Sifa za Mwombaji

Kuajiriwa mwenye Shahada ya kwanza ya Uhasibu au Fedha. Wenye uwezo wa kutumia Kompyuta na program kama Tally, QuickBooks na mifumo mingine zaidi. Wenye kuwa na maadili mema na historia safi ya kiutendaji na usimamizi wa fedha. Aidha, mwenye uzoefu wa angalau miaka mitatu (3) katika fani ya uhasibu watapewa kipaumbele.

#### 1.3 Ngazi ya Mshahara

EWSS-A KUANZIA TZS 800,000.

### 2.0 Mhandisi wa Ujenzi/Majengo (Civil/ Structual Engineer ) daraja la IA– Nafasi 2

#### 2.1. Majukumu ya Kazi.

(i) Kusimamia na kufanya ukaguzi wa Barabara, Madaraja na Majengo mbalimbali

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za ujenzi wa Barabara na Majengo

(iii) Kutayarisha bajeti kwa kila mradi wa Ujenzi na matengenezo ya Barabara ,Madaraja na Majengo yanayotekelezwa na kampuni.

(iv) Kusimamia na kuratibu kazi za Barabara/Madaraja na Majengo zinazotolewa na Serikali.

(v) Kuandaa tarifa za utekelezaji wa miradi kwa robo na mwaka

### 2.2. Sifa za Mwombaji

(i) Kuajiriwa wenye Shahada/Stashahada ya Juu ya Uhandisi (Bachelor of Science in Structual Engineering) kutoka katika Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali

(ii) Kuajiriwa wenye Shahada/Stashahada ya Juu ya Uhandisi (Bachelor of Science in Civil Engineering) kutoka katika Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali

(iii) Wenye uzoefu usiopunga miaka mitatu (3) katika fani ya Uhandisi wa Barabara.

### 2.3 . Ngazi ya Mshahara

EWSS-A KUANZIA TZS 800,000.

## 3.0 Masharti ya Jumla

(i) Waombaji wote wawasilishe barua za maombi ya kazi zilizoandikwa kwa mkono kwa lugha ya Kiingereza. Wawe ni Raia wa Tanzania umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 50.

(ii) Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.

(iii) Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya taaluma vinavyohusiana na nafasi husika. Pamoja na nkala ya kitambulisho cha NIDA.

(iv) Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).

(v) Picha moja ya rangi ya pasipoti iliyopigwa hivi karibuni.

**Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 15/08/2026**.

**Zingatia**

**Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (EWS Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; http: http://ews.sc.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Shule kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'EWS Recruitment Portal')**

**MENEJA WA SHULE,**
**ELLEN WHITE SCHOOL,**
**S.L.P 3118, DODOMA.**